**OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA OR – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE**

**Barua zote ziandikwe kwa Mkuu wa Shule**

**Email:** info@kikaro.sc.tz
**Email:** **emmyjkn@gmail.com**
**Website:** **www.kikaro.sc.tz**
**SIMU:0789021005/0784587853**

**Kumb: Na. KSS/Admn/vol- /2023.**

**Mkuu wa Shule,**
**Shule ya Sekondari Kikaro**
**S. L. P 48, CHALINZE**
**JUNE/2023**

JINA LA MWANAFUNZI ………………………………………………………………

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO**

**SHULE YA SEKONDARI KIKARO MWAKA 2023/2024**

Kichwa cha habari hapo juu chahusika:

Uongozi wa shule ya sekondari kikaro inafurahi kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule ya sekondari kikaro karibu.

Nafurahi kukufahamisha kuwa ,umepangiwa mchepuo wa **CBG/ HGL/ HGK/HKL** ( Kata isiyostahiki). Natumia nafasi hii kukupongeza kupata nafasi hii adhimu ambayo wengi wanaitamani na wameikosa. Bila shaka hutaipoteza “HONGERA SANA”. Unatakiwa kufika shuleni ***TAREHE 14 Agosti 2023 .***

Shule ya Sekondari Kikaro ipo mkoa wa **Pwani,** Halmashauri ya Chalinze katika kata ya Miono. Ukitoka Dar es salaam, panda magari yaendayo ***Saadani au Miono*** katika kituo cha daladala cha ***MBEZI YA KIMARA*** nauli ni Tsh 9,000/=. Ukitokea barabara ya **Arusha, Kilimanjaro na Tanga** unatakiwa kushuka kituo cha **Mandera Kibaoni** kabla ya kuvuka mto Wami**.** Hapo utapanda gari nyingine kwa nauli Tsh 2000/= au pikipiki kwa Tsh 5000/= tu na wakufikishe **Shule ya Sekondari Kikaro**. Ukitokea barabara ya Morogoro ( hasa kwa wanaotokea mikoa ya Rukwa, Mbeya, Iringa, Dodoma, Singida, Shinyanga n.k) utashukia kituo cha **Chalinze** kisha utakwenda stendi ya Tanga na utapanda gari nyingine zinazoelekea **Miono** kwa nauli ya shilingi 5000/= tu.

**HAKIKISHA UNAKUJA NA VITU VIFUATAVYO:**

1. Nakala ya matokeo ya kidato cha nne (result slip)
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
3. Fomu ya kuchaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano 2023/24 **iliyojazwa kikamilifu**.

**KUMBUKA:**

a. Fomu ya kupima Afya yako (iwe na muhuri wa Mganga Mkuu wa Mkoa/ Wilaya au Kituo cha Afya)
**b.** Hakikisha unawasilisha nakala na fomu iliyojazwa kikamilifu **siku ya kuripoti** ili kuepusha usumbufu.

Mkuu wa shule na wafanyakazi wengine wote wa shule hii wanakutarajia uwe mwanafunzi mtiifu, mwaminifu, nadhifu na mshiriki wa kazi zote za nje na ndani ya darasa.

**ANGALIZO**: Hakikisha unafika shuleni ndani ya wiki ya kwanza ya kufungua shule na si vinginevyo

THE HEADMASTER
KIKARO SEC. SCHOOL
P. O. Box 48, CHALINZE

**EMMANUEL JOHN KAHABI.**
**MKUU WA SHULE.**

FOMU NA. 01

**HALMASHAURI YA CHALINZE**

---

ANWANI YA MZAZI/MLEZI ,

S . L .P ……………………………………….

SIMU……………………………………….

TAREHE …………/……/20 …..

MKUU WA SHULE,

S.L.P 48,

CHALINZE.

YAH: **<u>UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO 2023/2024 SHULE YA SEKONDARI KIKARO</u>.**

---

**<u>SEHEMU A: (IJAZWE NA MWANAFUNZI)</u>**

Mimi (jina kamili ) ……………………………………………………………………….…… (Tahasusi …….……) niliyezaliwa tarehe ……………… Mwezi……………...... Mwaka ……………… Dini ………………………………..katika Kijiji cha ………………………….. Wilaya ya……………………………….. Mkoa wa…………………………………………

Nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha tano ***Shule ya Sekondari Kikaro***. Pia nitatii sheria na miongozo yote ya shule ambayo mwanafunzi anatakiwa kutekeleza hususani kufaulu vizuri na kutomiliki simu shuleni.

SAHIHI YA MWANAFUNZI …………………………………………………TAREHE ……………………………….

**<u>SEHEMU B: (IJAZWE NA MZAZI/ MLEZI)</u>**

Mimi …………………………………………………………….. (Jina kamili) wa Kijiji/Mtaa ....................................................... kata ya ……………………………………..Wilaya ya …………………………………Mkoa wa ……………………………………Dini……………………….……

Kazi yangu ni ……………………..

Nafurahi sana kupokea nafasi aliyopewa mwanangu. Nitatekeleza na kutimiza maagizo yote ya mtoto wangu kulingana na maagizo ya shule. Pia nitakuwa tayari wakati wote kusaidiana na shule katika kumlea mtoto huyu kitaaluma, kinidhamu na kimaadili na **kamwe hatomiliki simu akiwa shuleni** na ikitokea amekamatwa na simu afukuzwe shule kwa mujibu wa sheria.

SAHIHI YA MZAZI/ MLEZI ………………………………………………. TAREHE ……………………………………..

**<u>SEHEMU C: (IJAZWE NA AFISA MTENDAJI WA KIJIJI/MTAA/ KATA)</u>**

JINA…………………………………………………………………….. SAHIHI …………………………………….
TAREHE……………………………………………….. MUHURI……………………………….

FOMU NA: 2

## HALMASHAURI YA CHALINZE

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI KIKARO,
S.L.P. 48.
…. /…. /202…

MGANGA ………………………………….
HOSPITAL/KITUO CHA AFYA ……………………
S L . P ……………………

### YAH: <u>KUPIMA AFYA (MEDICAL EXAMINATION)</u>

Tafadhali mpime mwanafunzi …………………………………………………………………….

Kama afya yake inamruhusu kuendelea na masomo ya Sekondari kidato cha Tano mwaka 2023/24 Andika

NDIYO au HAPANA katika nafasi zilizoachwa wazi mbele ya ugonjwa kama aliugua.

1. Kifua Kikuu ………………………………………
2. Ugonjwa wa moyo ………………………………………
3. Ugonjwa wa figo ………………………………………
4. Ugonjwa wa akili ………………………………………
5. Ajali kubwa ………………………………………
6. Pumu…………………………………………….
7. Vidonda vya tumbo ……………………..….
8. Kifafa …………………………………………
9. Kupasuliwa ………………………………….
10. seli mundu ……………………………

10. Mengineyo

………………………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………………………

<u>MAELEZO YA MGANGA</u>

…………………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………………… JINA LA

HOSPITALI /KITUO CHA AFYA ………………………………………………………………

JINA MGANGA…………………………………………… SAHIHI ………………………………………

TEREHE ………………………………………. MUHURI …………………………………

**SARE YA SHULE NA MAHITAJI MENGINE;**

i. Suruali za **dark blue (02)**, **ZIWE NA MARINDA MAWILI**, zenye upana wa inchi **18’’** (**wavulana**) huvaliwa darasani
ii. Suruali za **nyeusi mbili (02)**, zenye upana wa inchi **18’’** (**wavulana** ) huvaliwa baada ya muda wa darasani
iii. Mashati meupe **mikono mirefu** mawili **(02)** kwa **wavulana na wasichana.Kwa wasichana wa kiislamu wanaweza kushona nusu kanzu ambayo itafanana na juba jeupe la darasani.**
iv. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba vyenye visigino vifupi jozi mbili **(02)** (**wavulana na wasichana**)
v. **Wavulana** huvaa **tai rangi dark blue** na **wasichana** huvaa **skafu dark blue .**
vi. Sketi mbili ndefu hadi chini, (**mshono wa rinda box**) rangi ya **dark blue** kwa **wasichana** – huvaliwa darasani
vii. Sketi mbili ndefu hadi chini **rangi nyeusi** za rinda box kwa ajili ya kushindia (**wasichana**)
viii. T – Shirt (02) **zenye nembo ya shule** ambazo **huvaliwa darasani** kila siku ya **Jumatano** na **Ijumaa**.
ix. T – Shirt (02) za kushindia na **zenye nembo ya shule** baada ya muda wa darasani.
x. Truck suit rangi ya dark blue yenye **jina la shule**.
xi. **Shuka mbili** (cotton) za **blue bahari** kwa **wavulana** na rangi ya **pinki** kwa **wasichana**
xii. **Sweta rangi ya dark blue** hasa kwa wale wenye **matatizo ya kifua/upumuaji**.
xiii. Kila mwanafunzi ni lazima aje na **nguo za michezo**, **wavulana** waje na **jezi nyeusi ya Taifa stars** jozi moja na **wasichana** waje na **jezi nyeupe ya Taifa stars** jozi moja.
xiv. Kila mwanafunzi ni lazima aje na **viatu vya michezo** (**wavulana raba nyeusi** na **wasichana raba nyeupe**)
xv. Kanga /kitenge jozi moja, taulo pamoja na nguo halisi za kulalia kwa **wasichana**
xvi. **Sanduku la bati na kufuli lake** kwa ajili ya kuhifadhia vitu vyake.
xvii. **Godoro moja futi mbili na nusu kwa sita** lenye ujazo wa inch 4 ( 2½ x 6 x 4’’) .
xviii. Kila wanafunzi ni lazima aje na chandarua (**nyeupe** kwa **wasichana** na **blue** kwa **wavulana**)
xix. **Kontena,kijiko, kikombe** na **ndoo (02) za lita kumi** kwa ajili ya matumizi binafsi na **dumu moja** la kuhifadhia maji ya kunywa la lita 20
xx. **Kila mwanafunzi ni lazima aje na RIMU mbili nyeupe za karatasi A4 pindi anaporipoti shuleni.**
xxi. <u>**Kwa mabinti wa kiislamu**</u>**:**
   - **Juba mbili nyeupe** kwa ajili ya darasani urefu hadi kwenye vifundo vya mikono na **Juba mbili nyeusi** kwa ajili ya kushindia urefu hadi kwenye vifundo vya mikono
   - Vitambaa (vikofia) vya kuvaa **ndani ya juba** viwe rangi **nyeupe** au **nyeusi** tu.

xxii. Vifaaa vifuatavyo kila mwanafunzi avilete kutokana na tahasusi yake:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **CBG** | Hard broom - **moja** | Toilet brush - **moja** | Fyekeo (kwanja)- **moja** |
| **HGL** | Soft broom - **moja** | Squeezer- **moja** | Fyekeo (Kwanja) - **moja** |
| **HGK** | Ufagio wa cherewa za mti - **moja** | Squeezer- **moja** | Fyekeo (kwanja) - **moja** |
| **HKL** | Hard broom - **moja** | Soft broom- **moja** | Jembe - **moja** |

- Hairuhusiwi kwa mwanafunzi yeyote kuja na mapambo, urembo, mafuta yenye harufu kali au manukato ya aina yoyote.
- Mwanafunzi yeyote mwenye matatizo ya kiafya aje na taarifa kutoka hospitali inayotambulika na serikali.
- **KILA MZAZI AHAKIKISHE ANAMKATIA MTOTO WAKE BIMA YA AFYA YA NHIF.**

**MICHANGO MBALIMBALI YA SHULE KWA SHULE ZA BWENI**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

- Michango yote ni lazima ilipwe Benki ya NMB.
  ***JINA LA AKAUNTI: KIKARO SECONDARY SCHOOL.***
  ***AKAUNTI NA: NMB 21101100021***
  **TAWI LA BENKI: NMB CHALINZE**
- **Malipo yote yafanyike kupitia akaunti ya shule na sio vinginevyo.**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahtuti hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

**MAWASILIANO**

- **Mkuu wa shule**: 0789021005
- **Makamu Mkuu wa Shule**: 0788 776 331 au 0784587853
- **Taaluma**: 0782743206 au 0676821985
- **Malezi na Nidhamu (Mapokezi)** 0688509008 **,** 0783505171 na 0764718417 Kwa maelekezo zaidi tafadhali tembelea Tovuti ya shule : www.kikaro.sc.tz

**E-**mail: info@kikaro.sc.tz

**MAWASILIANO YA MZAZI NA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI YATAFANYIKA KUPITIA NAMBA HIZI.**

- **WANAFUNZI WASICHANA: MATRON** 0782444970, MWL 0789400229, MWL 0686121912
- **WANAFUNZI WAVULANA : PATRON** 0785480658, MWL 0783835563, MWL 0682836468

**Wanafunzi wa Mchepuo wa CBG Wanatakiwa kuja na vitu vifuatavyo**.

- ***Dissecting kit (0ne set)***
- ***White laboratory coat***
- ***Non programmable Calculator***

## 3.1 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Vilevile katika jamii ni lazima kuwepo na sheria na kanuni ili kila mmoja aishi katika hali ya amani, usalama na utulivu. Aidha ili kuona kuwa kila mmoja anatendewa haki.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shule ya sekondari Kikaro.

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule kama zilivyoanishwa kwenye mahitaji ya wanafunzi na si vinginevyo.
2. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria shuleni na kufuata ratiba iliyowekwa
3. Mwanafunzi anatakiwa kuwa mtulivu na mkimya wakati wote anapokuwa darasani, mistalini na wakati wa kulala. Pia anatakiwa kuwepo darasani wakati wote kama hajaruhusiwa kutoka njee na kiongozi wa darasa au mwalimu.
4. Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au mwanafunzi na mwalimu ni ya lugha ya kiingereza na si vinginevyo
5. Mwanafunzi anatakiwa kukaa shuleni wakati wote wa shule na ni marufuku kuvuka eneo la shule bila ruhusa ya maandishi ya mwalimu wa zamu patron au matron ;

    **i.** Ni marufuku kwa mwanafunzi kutoka nje ya MIONO bila ya ruhusa **ya MWALIMU WA MALEZI, MAKAMU MKUU WA SHULE NA MKUU WA SHULE**

    ii. Wageni wote wafike ofisi ya malezi au matron kabla ya kuonana na mwanafunzi husika

    iii. Wanafunzi wa hostel watatembelewa jumapili ya mwisho wa mwezi tu

    iv. Wanafunzi wa hostel wataenda sokoni kila jumatano ya mwisho wa mwezi baada ya masomo.

6. Kila mwanafunzi anatakiwa kuonesha heshima ya hali ya juu kwa ;

    i. Kumsalimia kila mtu anayemzidi umri

    ii. Kupokea mzigo mwalimu au mgeni.

    iii. Kutii bendera taifa kwa kusimama na kukaa mguu sawa inapopandishwa au kushushwa kwa mwongozo wa filimbi au mimbo wa taifa.

    iv. Kutii wimbo wa Taifa unapoimbwa

    v. Kuwaheshimu viongozi wa serikali ya wanafunzi

    vi. Ni kosa kutoa kauli chafu au matusi, kupigana na kukashifiana na mwanafunzi mwenzio au mwalimu.

7. Kila mwanafunzi lazima awe nadhifu wakati wote ndani ya eneo la shule na nje ya shule. Ni marufuku kuvaa sketi fupi, nguo za kubana mwili, na ni kosa kuvaa kofia eneo la shule.
8. Ni jukumu la kila mwanafunzi kuhakikisha kuwa anatimiza wajibu wake kwa kushiriki kikamilifu katika kazi zote za elimu ya kujitegemea na utunzaji wa mzingira. Ni kosa kuharibu mazingira kwa kutupa karatasi ovyo, kuchoma moto na kukatiza kwenye viunga.
9. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa mwaminifu na mtunzaji wa mali za umma, pia ni kosa kusema uongo, kuiba na kuficha maovu.
10. Hairuhusiwi msichana kuingiza mvulana au mvulana kuingiza msichana bwenini.
11. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
12. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**KUMBUKA.**

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele.Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KIKARO**

***"KIKARO BILA DIVISHENI THREE INAWEZEKANA"***

THE HEADMASTER
KIKARO SEC. SCHOOL
P. O. Box 48, CHALINZE

EMMANUEL JOHN KAHABI

**MKUU WA SHULE**